# SHULE YA SEKONDARI DODOMA

**S.L.P 32,DODOMA.**
**Baruapepe:** *dodoma.sec@dodomacc.go.tz*
**Simu :** 026 – 2321163 **Simu:** 0784531333

Kwa mzazi/mlezi wa: ……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DODOMA KIDATO CHA TANO (V) MWAKA ...................**

## 1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Dodoma kidato cha Tano mwaka …………… kwa tahasusi ya …………... Shule itafunguliwa tarehe …………………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………………... Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………….

## 2.0 KUFIKA ILIPO SHULE:

Shule ipo umbali wa kilometa nane kutoka kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani (Nanenane). Unaweza kufika shuleni kwa kutumia daladala ziendazo Sabasaba kwa nauli ya Tsh 800/= Shule ipo jirani kabisa na kituo cha daladala cha Sabasaba na inapakana na kituo cha afya Makole, upande wa Magharibi na majengo ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania upande wa Kusini Mashariki.

## 3.0 MAMBO MUHIMU YA KUFANYA

Pamoja na kufanikiwa kupata nafasi hii muhimu ya kujiunga na kidato cha Tano, nakusisitiza mambo yafuatayo:-

a) **Kusoma kwa makini** maelezo yote yaliyoko katika fomu hii ya kujiunga (Joining Instructions) ya shule hii na kutekeleza bila kisingizio maelekezo yote ili kuleta ufanisi wenye tija katika kukupatia elimu iliyo bora kwa muda wote wa masomo.

b) Dodoma Sekondari ni shule ya Bweni kwa ajili ya **wasichana wote kidato cha Tano na Sita tu (hatuna nafasi ya kutwa kwa vidato tajwa)**.

c) Kujaza fomu Na: 1, 2 na 3 na kuzirudisha shuleni wakati wa kuripoti. Fomu na.3 ijazwe na daktari wa **hospitali au kituo cha afya cha serikali**. Fomu zote zibandikwe picha za pasipoti size kama zinavyoelekeza.

## 4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 4.1 AFYA

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni na kadi ya bima ya afya (NHIF) na kama hana atatakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya na kupata kadi kwa gharama ya **Tsh.50,400/= kwa mwaka** mara anaporipoti shuleni.

b) Kila mwanafunzi lazima apimwe afya yake kabla ya kujiunga na shule na wakati wowote shule itakapoona kuna haja na umuhimu wa kufanya hivyo.

c) Endapo mwanafunzi ataugua ataomba kibali kwa mwalimu mlezi (matron) na kwenda hospitali na kurudi siku hiyo hiyo. **Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na Mkuu wa Shule pekee.**

d) Mwanafunzi mwenye tatizo la kiafya kama vile pumu, moyo, kifua kikuu n.k lazima tatizo lake lithibitishwe na daktari wa hospitali ya serikali ambaye atamshauri mgonjwa na shule kwa maandishi.

e) Kila mwanafunzi anatakiwa kula chakula cha shule mesini au maeneo yaliyoruhusiwa na shule. Hairuhusiwi mwanafunzi kula chakula nje ya maeneo yaliyoruhusiwa kama vile bwenini au darasani.

f) Kila mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake na kuwa safi wakati wote kwa kukata kucha, kutopaka kucha rangi/ina, kuoga, kusafisha meno, kutandika kitanda na kupanga vitu vizuri bwenini. Hairuhusiwi kuvaa pete, ‘culture’, shanga,mikufu, hereni na mapambo mengine ya mwilini.

### 4.2 SARE YA SHULE

a) Sare ya shule iliyo sahihi kwa wasichana,ni sketi ndefu inayofika kwenye vifundo vya miguu (**ankle**) ya rangi ya **blue nyeusi** (**Dark blue**) ya marinda ya kupanga yenye upindo (belt) wa inchi mbili, isiyo na mikanda (zinapatikana karibu na duka la shule kwa bei ya Tshs. 27,000/=)

b) Shati jeupe mikono mifupi, lililoshonewa namba tano ya kirumi **V** kwenye mabega yote mawili (kwa kutumia kitambaa cha sketi) itakayosomeka kwa mbele. Mzazi anashauriwa kumnunulia mwanae jozi mbili (2) za sare ya shule. (kwa atakayehitaji kununua shuleni zinapatikana karibu na duka la shule kwa bei ya Tshs. 15,000 kila moja**)**

c) Wanaovaa hijabu mashati yao ni mikono mirefu na **hijabu nyeupe** isiyo na urembo wa aina yoyote ya kuvaa sambamba na sare ya shule na sio vilemba au mitandio. Ni muhimu kuhakikisha hijabu inafunika kifua sambamba na viwiko vya mikono (kwa atakayehitaji kununua shuleni anaweza kupata katika duka lililo karibu na shule kwa bei ya Tshs. 15,000/=

d) Viatu vya rangi nyeusi vya **kufunga na kamba** na visiwe na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili (kwa atakayehitaji

kununua shuleni vinapatika karibu na dula la shule kwa bei ya Tshs. 25,000/=).

e) Viatu vijulikanavyo kama 'simple' vyenye kuacha sehemu ya miguu wazi haviruhusiwi kabisa kuvaliwa shuleni.

f) Nguo za michezo ni Tracksuit ya rangi ya **Dark blue** (yenye mistari myeupe ubavuni) isiyo na maandishi, raba nyeusi na soksi za blue. **(kwa atakayehitaji kununua shuleni zinapatikana katika duka karibu na shule kwa bei ya Tsh. 30,000/= kila moja).**

g) Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

h) Sweta la **blue mtindo wa V - shingoni** kwa ajili ya kuvaa wakiwa darasani (**kwa atakayehitaji kununua shuleni Masweta yanapatikana karibu na dula la shule kwa bei ya Tsh.15,000/= kila moja**). N.B Sweta litavaliwa kipindi cha baridi pekee.

**Zingatia**: **Mzazi unashauriwa kumfungulia akaunti ya benki (bank account) mtoto wako, uongozi/watumishi wa shule hawatohusika kupokea fedha yoyote kupitia simu.**

**MAHITAJI MUHIMU YA BWENI/HOSTEL**

a) Wanafunzi wa Bweni awe na jozi mbili za sketi ndefu**, inayofika** kwenye vifundo vya miguu (**ankle) za rangi nyeusi** zenye upindo (belt) wa inchi mbili, zenye marinda ya kupanga na zisizo na mikanda (zinapatiakana karibu na duka la shule kwa bei ya Tshs. 27,000/=).

b) T- shirt ya **maroon** na T – shirt ya **kijivu** zenye nembo ya shule. **(kwa atakayehitaji kununua shuleni zinapatikana karibu na duka karibu na shule kwa bei ya Tsh.15,000/= kila moja)**

c) Suruali **nyeusi 2** pana zisizobana za kulalia na jaketi la **blue lisilo na maandishi** au urembo litavaliwa usiku wakati wa kujisomea (Preparation).

d) Shuka mbili na foronya mbili za rangi ya **light blue**, blanketi, Chandarua cha rangi nyeupe (white mosquito net) na mto.

e) Taulo 1 na nguo za ndani za kutosha.

f) Ndoo mbili nyeupe; 1 ya lita kumi na 1ya lita 20.

g) Godoro la futi 2.5 kwa futi 6, **(2.5 x 6 x 8")**;. (Cover unaweza ukaipata karibu na duka la shule kwa bei ya Tsh 45,000/=)

h) Vyombo vya kulia chakula (vya plastiki) kikombe na bakuli kubwa lenye vyumba vinne (rangi ya Light ya Pink) pamoja na kijiko.

i) Wanaovaa hijabu, watavaa **hijabu nyeusi** nje ya muda wakawaida wa madarasa sambamba na T-shirt za shule na si vinginevyo.

**ANGALIZO**

a) Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na Tranka moja tu na asilete shuleni nguo za ziada ambazo hazijaidhinishwa.

b) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni/wazazi wakati wote atakaokuwepo hapa shuleni ISIPOKUWA kwa wito maalumu iwapo italazimika.
Siku ya kuwaona wanafunzi ni siku itakayotangazwa na uongozi wa shule.

c) Ni muhimu kwa mzazi/mlezi kutoa ushirikiano kwa walimu katika malezi ya mwanafunzi.

**Zingatia Kielelezo cha sare za shule**



Mfano wa sare sahihi



Mfano wa sare sahihi kwa Mwanafunzi wa kiislamu



Uvaaji wa masweta kipindi cha baridi



Aina ya malinda na sehemu sahihi ya kuvalia sketi

Mfano wa Viatu vya gidamu vilivyofunika miguu





Mfano wa bakuri sahihi ya chakula

## 5.0 MICHANGO YA SHULE

a) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:-**

- Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho.
- Tsh 65,000/= uendeshaji wa shule
- Tsh 5,000/= nembo moja ya shule
- Fedha ya huduma ya kwanza Tsh.5,000/= (haitarejeshwa)

Malipo yote ni kupitia Benki ya NMB**;** namba **50501100160** yenye jina la**: Dodoma Secondary School Ruzuku.** Risiti zote za malipo (bank pay in slip) ziwasilishwe **Ofisi ya Uhasibu** na kupatiwa risiti. (Tafadhali hakikisha umepatiwa risiti baada ya kuwasilisha risiti yako ya malipo)

**ANGALIZO**: Shule haitahusika na malipo yoyote yatakayofanywa bila kupitia benki.

## 6.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI.

a) Begi jeusi la mgongoni kwa ajili ya kubebea daftari (begi lisiwe na mapambo yoyote).
b) Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo:- mfagio wa ndani 1 (soft bloom) na lita moja ya dawa ya chooni ya ARO au yenye ubora unaofanana nayo kwa ajili ya kufanyia usafi kwa ajili ya kufanyia usafi.
c) Wanafunzi wa CBG waje na reki 1, HGL waje na 'squeezer' 1 yenye mpini, PCM waje nafyekeo 1 na HGK brashi 1 ya kusugulia choo (toilet brush), PCB waje na hard broom 1, EGM waje na panga 1 na PMC's waje na USB flash drive za GB 16 .
d) Atatakiwa kuleta Rimu (2) za karatasi ya photocopy na sio Rulled wala Duplicating papers (kwa mwaka)
e) Vifaa vya kujifunzia vya kutosha kama vile daftari, graph pads 05, Kalamu, Vitabu na Scientific calculators kwa wanafunzi wa Sayansi na Hisabati (zinapatikana katika duka karibu na shule).
f) Wanafunzi wa Biologia CBG na PCB waje na seti ya Dissection Kit, tray na lab coat kwa ajili ya mazoezi ya upasuaji (Dissections). (zinapatikana katika duka karibu na shule).
g) Ieleweke kuwa **hairuhusiwi kuja na simu shulen**i/kutumia simu ya mtumishi yeyote asiyeidhinishwa na uongozi wa shule, na mwanafunzi atakayekamatwa na simu atafukuzwa shule.
h) Mwanafunzi atatakiwa kuleta picha za passport size tatu (3) akiwa na sare ya shule atakapokuwa ameripoti shuleni. (Andika jina na tahasusi nyuma ya picha). **Ikumbukwe kuwa muda wa mwisho kuripoti shuleni ni saa 12:00 jioni kwa wanaotoka mikoa ya mbali zaidi na Dodoma.**

## 7.0 SHERIA ZA SHULE

### 7.1 RATIBA YA SHULE.

Kila mwanafunzi azingatie kwa makini ratiba ya shule kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati muafaka. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa shuleni kuanzia saa moja kamili asubuhi kila siku kwa siku za masomo na kufanya yafuatayo:-

a) Kufanya usafi katika eneo lake alilopangiwa (special area)
b) Awahi mstarini (parade) na kuchukuliwa mahudhurio mapema kengele inapogongwa, wachelewaji watasaidiwa haraka] na walimu watakaokuwa zamu.
c) Kuingia darasani na kuhudhuria vipindi vyote kama vilivyo katika ratiba ya shule.
d) Ni lazima na sio hiari kwa mwanafunzi kufanya mazoezi yote yanayotolewa ndani na nje ya darasa.
e) Kutii na kuheshimu kengele kwa kuwa mahali panapohusika kwa wakati mwafaka.

### 7.2 MATUMIZI YA SARE ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi atatakiwa kuwa katika sare ya shule kama ilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule(Joining Instruction)
b) Wakati wa michezo wanafunzi wote watakuwa katika sare kamili ya michezo wakati wa ushiriki wao katika michezo na siyo vinginevyo.
c) Wanafunzi wa hosteli wawe na sare kamili wakati wakiwa nje ya madarasa
d) Kipindi cha baridi wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa sweta za **rangi ya bluu** yenye muundo wa **V** shingoni wakiwa shuleni, majaketi **hayataruhusiwa.**
e) Wanafunzi wa Bweni wavae sare kamili ya shule wanaposafiri kwenda likizo au wanaporudi kutoka likizo.

### 7.3 NIDHAMU

a) Hairuhusiwi mwanafunzi kutoka nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu, wanafunzi wa Bweni. Ruhusa ya kutoka nje ya shule itatolewa na matron, patron au Mkuu wa Shule.
b) Hairuhusiwi kukatiza uzio "tracepassing" katika njia isiyoruhusiwa, wanafunzi
c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuzurura nje wakati wa vipindi, wanafunzi watakaokuwa na private studies wanashauriwa kuwa maktaba, ukumbi au darasa maalum litakalotengwa kama ukumbi wa shule utakuwa na matumizi mengine.
d) Hairuhusiwi kwa wanafunzi kuja na simu za mkononi shuleni.
e) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele anapokuwa parade, darasani au bwenini.
f) Hairuhusiwi mwanafunzi kufuga, kucha, nywele na kusuka.
g) Mwanafunzi anapaswa kuwa nadhifu lakini haruhusiwi kutumia vipodozi kama wanja, lipshine/lip gross, eyeshadow, cream n.k.

h) Wanafunzi wawapo shuleni, matibabu yao yatafanyika katika hospitali za umma.

i) Mwanafunzi awapo shuleni hatoruhusiwa kutoka nje ya shule isipokuwa siku maalumu (outing day na kwa ruhusa maalumu)

j) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba kwa ufasaha nyimbo zifuatazo:-

- Wimbo wa "Taifa"
- Wimbo wa Afrika Mashariki
- Wimbo wa "Tanzania nakupenda"
- Wimbo wa "Shule".
- Wimbo wa "Tazama ramani"
- Wimbo wa "Kuwasha mwenge"

## 7.4 SEHEMU AMBAZO WANAFUNZI HAWARUHUSIWI KUFIKA BILA KIBALI

- Chumba cha walimu (Staff room)
- Maabara
- Ofisi ya shule
- Jikoni
- Nyumba za walimu na wafanyakazi

## 7.5 SEHEMU ZILIZOPIGWA MARUFUKU WANAFUNZI KUTEMBELEA.

- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe (Clubs)
- Nyumba za kulala wageni.

## 7.6 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

Makosa yaliyoorodheshwa hapa chini yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule moja kwa moja.

a) Wizi.
b) Kutohudhuria shule masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
e) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote

f) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
g) Kufuga ndevu.
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
i) Uvutaji wa sigara.
j) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa.
k) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
l) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
n) Kumiliki, kukutwa au kutumia kadi ya simu au simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
o) Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
p) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
q) Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi ikiwemo kuchora/kuandika ukuta, kuharibu mabomba, viti au meza.
r) Kukataa adhabu kwa kudharau au kwa kiburi
s) Kukutwa nje ya shule bila ruhusa au kibali (Utoro)

......................................

**FRANCIS W. TUMAINI**

**MKUU WA SHULE**

# FOMU NA. 1: AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi ......................................................wa S.L.P.................Mji. ............................Simu Na...........................Ambaye kazi yangu ni ....................................... natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ...........................................................Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya Sekondari Dodoma kuanzia tarehe ..............................Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa maswala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina..............................................saini...............tarehe..............Uhusiano na mwanafunzi................................

---

# AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ......................................................Wa kidato cha Tano chaguo ..................... (tahasusi) mwaka 2017 / 2018.Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Dodoma. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na taifa langu.

Jina..............................................saini.......................Tarehe.................

**Maoni ya Mkuu wa Shule**

.......................................................................................................................
.......................................................................................................................
.......................................................................................................................

# FOMU NA. 2: KIAPO CHA MZAZI / MLEZI

Mimi…………………………………………wa………………S.L.P. …….Mji……………………….. Simu Na……………………Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu wanne(4) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:- (ambatanisha picha passport size zao)

1\.

Jina…………………………………………………………………………

Simu………………………………………… uhusiano…………………

2\.

Jina ………………………………………………………………………..

Simu……………………………………… uhusiano………………..

3\.

Jina…………………………………………………………………………

Simu……………………………………….. uhusiano………………..

4\.

Jina ……………………………………………………………………..

Simu…………………………………… uhusiano………………..

Saini ya mzazi / mlezi……………………………Simu……………………Tarehe:……………………

# FORM NA. 3: UTHIBITISHO WA AFYA

Dodoma Secondary school
P.O. BOX 32
DODOMA.

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name ……………………..…………………..Age……...Sex………..year……………

1. Blood count (Red and White) …………………………………………………...
2. Urine analysis Test …………………………………………………………….
3. Syphilis test ……………………………………………………………………….
4. T.B. ……………………………………………………………………………………..
5. Eye Test …………………………………………………………………………….
6. Ears ……………………………………………………………………………………
7. Spleen ………………………………………………………………………………
8. Abdomen ……………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

| | |
|---|---|
| ……………………………….. | ……………………………………. |
| Name and Designation | Signature and Official stamp |
| ……………………………….. | ……………………………… |
| STATION | DATE |

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.